# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI


Barua pepe

SHULE YA SEKONDARI
Namba za Simu
**Mkuu wa Shule**
0762773954/0627812420
**Makamu Mkuu wa Shule**
0746420986
**Matroni**
0768186713

mizengopindasec@gmal.com
MIZENGO PINDA,
S.L.P 607,
MPANDA – KATAVI.


Mzazi/ Mlezi wa……………………………………………
S.L.P ………………………………………………………….
…………………………………………………………………….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA
MWAKA WA MASOMO 2021/2022

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka wa masomo 2021/2022, tahasusi ya …………….. Shule ya sekondari **Mizengo Pinda** ni ya bweni na ni ya wasichana. Shule ipo umbali wa kilomita 110 Kusini magharibi mwa mji wa Mpanda. Shule iko karibu na **CHUO KIKUU CHA KILIMO CHA SOKOINE (SUA) CAMPUS YA MIZENGO PINDA** kilichopo Mkoa wa Katavi. Usafiri wa basi kutoka **Mjini Mpanda** unapatikana katika kituo cha **mabasi Mpanda**, nauli ni shilingi elfu nane (TSh. 8,000/=) hadi eneo la KIBAONI. Kwa wanaotokea **Dar es Salaam** wanaweza kupanda mabasi ya kwenda **Mbeya au Sumbawanga** moja kwa moja. Wakifika Mbeya watapanda mabasi ya kwenda Sumbawanga na wakifika Sumbawanga watapanda mabasi ya kwenda Majimoto na kushuka kituo cha **KIBAONI.** Kwa wanaotokea **mikoa ya Kilimanjaro na Arusha** watapanda mabasi yanayokwenda **Mpanda** kupitia Mkoa wa Tabora na kushuka **Mpanda Mjini. Usafiri wa basi kutoka Mpanda Mjini hadi kituo cha mabasi eneo la Kibaoni unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda, nauli ni shilingi elfu nane (TSh. 8,000/=). Ukiwa mjini Mpanda utapanda mabasi ya kwenda Majimoto na kushuka Kibaoni**. Kwa wanaotokea **Mwanza** watapanda mabasi yanayokwenda Sumbawanga kupitia Tabora Mjini na basi litaendelea na safari kupitia Inyonga, Majimoto na utashuka kituo cha mabasi **KIBAONI. Kutoka KIBAONI** hadi shule ilipo ni umbali wa mita 700 tu ama unaweza kuchukua pikipiki (bodaboda) hadi shuleni kwa nauli yake ni shilingi elfu moja (TSh. 1,000) tu au waweza kuja kwa miguu.

   Tafadhali wahi kufika maana ukichelewa zaidi ya wiki moja (1) nafasi itachuliwa na mwanafunzi mwingine. Wanafunzi watapokelewa kuanzia tarehe **03/07/2021** Pamoja na maagizo mengine, mwanafunzi anapaswa kuja na **Result slip (original) ya matokeo ya kidato cha Nne 2020**.

   Hongera kwa kuchaguliwa katika shule hii, nakutakia maandalizi mema na safari njema.

ALICKO J. KAMINYOGE
MKUU WA SHULE

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. KARO NA MICHANGO

| Na. | AINA YA MALIPO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | ADA (inaruhusiwa kulipa nusu yaani 35,000/= kwa kila muhula) | 70,000/= |
| 2 | UKARABATI WA SAMANI | 15,000/= |
| 3 | KITAMBULISHO NA PICHA | 6,000/= |
| 4 | TAALUMA | 20,000/= |
| 5 | KUWALIPA VIBARUA (Wapishi, walinzi na vibarua wengine) | 30,000/= |
| 6 | HUDUMA YA KWANZA | 5,000/= |
| 7 | BIMA YA AFYA | 5,000/= |
| 8 | MITIHANI YA MOCK | 20,000/= |
| 9 | FEDHA YA TAHADHARI (ambayo haitarejeshwa) | 5,000/= |
| 10 | UMEME | 12,000/= |
| JUMLA | | 188,000/= |

Pamoja na michango ya TShs 188,000/= mwanafunzi aje na ream mbili za karatasi za A4.
Ada na michango mingine (**isipokuwa fedha ya huduma ya kwanza na bima ya afya**) iingizwe katika akaunti ya shule iliyopo katika Benki ya NMB (Account No. 61901200077 inayoitwa MIZENGO PINDA SEC CAPITATION ACC) kisha tuletee *Bank pay–in-slip* ukiwa umeandika jina lako na mchanganuo wa malipo nyuma ya karatasi hiyo.

B. SARE ZA SHULE

(i) Sare za darasani Sketi mbili, kati ya hizo moja iwe ya rangi ya orange (karoti) na nyingine iwe ya rangi ya ugoro kitambaa aina ya esteem original no 1. Sketi zote ziwe na linda box, linda 8, linda moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande wa kushoto (SKETI ZIWE NDEFU SANA ZIFIKE KWENYE KIFUNDO (ANKLE) CHA MIGUU YA MWANAFUNZI NA SI VINGINEVYO. SKETI FUPI HAZITAKIWI KABISA NA HAZITAPOKELEWA. **Sare hizi unaweza ukashona mwenyewe na kuja nazo. Unashauriwa kushona shuleni ili ziwe na mfanano katika mshono na rangi lengwa.**

(ii) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu na yasiyo na urembo wowote. **Aje nayo.**

(iii) Sweta la shule rangi ya ugolo lenye nembo ya shule. **Linapatikana shuleni**

(iv) Sare ya kushindia (Shamba dress) ni rangi ya pink iliyokolea aina ya Esteem original no 1, Iwe ya linda box, linda 8, linda moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande wa kushoto (SKETI ZIWE NDEFU ZIFIKE KWENYE KIFUNDO (ANKLE) CHA MIGUU YA MWANAFUNZI (SKETI FUPI HAZITAKIWI NA HAZITAPOKELEWA). **Sare hizi unaweza kuja nazo au utashona shuleni**.

(v) T-shirt mbili rangi ya kijivu na kijani kibichi zenye nembo ya shule. **Zinapatikana shuleni.**

(vi) Track suit jozi moja (rangi moja ya koti, T- shirt na suruali) rangi ya kijivu yenye

mistari myeupe pembeni (grey plain). **Aje navyo**

(vii) Kiatu cheusi cha ngozi chenye Kamba na kisigino kifupi pair moja kisiwe na urembo wa aina yoyote. **Aje nacho**

(viii) Kiatu Raba nyeupe yenye kamba pair moja isiwe na urembo wa aina yoyote. **Aje nayo**

(ix) Soksi nyeupe jozi mbili zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi. **Aje nazo**

(x) Wanafunzi wa kiislamu washone nusu kanzu nyeupe mbili ambazo ni ndefu hadi katikati ya paja ikiambatana na hijabu nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua. **Aje nazo**

**NB: Si jukumu la shule kushona sare za wanafunzi, Mwanafunzi mhusika ataelekezwa kwa mtu aliyeteuliwa na shule kwa kazi hiyo, utaratibu huu umewekwa ili wanafunzi wawe na sare zinazofanana. Hivyo jumla ya gharama ya sare zote zinazopatikana shuleni ni Tsh. 115,000/= aje nazo mkononi, atakabidhiwa fundi.**

C. SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:

(a)Masomo darasani
(b)Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
(c)Baraza la shule
(d)Kwenda hospitalini
(e)Kwenda maandamano
(f)Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo
(g)Kazi za mikono (vazi la kazi)
(h)Michezo

**NB**: Mwanafunzi huruhusiwi **kuja na nguo za nyumbani** Nje ya zile ulizo agizwa na shule

D.VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA NA VINAWEZA KUPATIKANA KARIBU NA SHULE

Mwanafunzi anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo;

VIFAA VYA USAFI

Kwanja 1, Jembe 1 lenye mpini, reki 1, Brush ngumu 1, Mfagio wa ndani 1, mfagio wanje1, Panga nzito 1, na ndoo mbili kubwa za plastiki.

VIFAA VYA DARASANI

i. Angalau daftari 8 za counter books Quire 3 au 4
ii. Rula moja ya sentimita 30
iii. Kalamu za wino na za risasi za kutosha
iv. Faili la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi
v. Mathematical seti 1

MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA MWANAFUNZI

i. Godoro la sponji $2^1/_2$ x 6
ii. Chandarua rangi nyeupe
iii. Shuka mbili za rangi ya pinkK zisiwe na maua au urembo wowote
iv. Mto na foronya rangi ya pink
v. Tochi/ taa ndogo ya solar kwa ajili ya dharura
vi. Blanketi moja rangi yoyote
vii. Shuka nzito rangi yoyote
viii. Taulo moja au mbili rangi yoyote
ix. Doti moja au Mbili za khanga au kitenge rangi yoyote

x. Kandambili kwa ajili ya kuogea
xi. Awe na sanduku/Tranka linalofunga vizuri kwa kuhifadhia vitu vyake
xii. Alete Pasport size tatu (03) zilizopigwa kwenye kitambaa cha blue bahari avae shati la shule(nyeupe) kwa ajili ya kuweka kwenye faili litakalo hifadhia nyaraka za mwanafunzi.

VIFAA VYA CHAKULA

i. Sahani, Bakuli na kijiko
ii. Kikombe

VIFAA VYA MICHEZO

Raba za michezo, T-shirt ya bluu ya michezo na bukta ya bluu ya michezo.

E.1. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama Ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote Inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na mafunzo ya Ufundi yenye dhamana nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.
Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yatakayofafanuliwa zaidi utakafika Shuleni:

a) Utatakiwa kuwaheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
b) Utatakiwa kuwa na mahudhurio mazuri katika kila shughuli inayofanyika ndani au nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
c) Utatakiwa Kushirki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Utatakiwa Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Utatakiwa Kufahamu mipaka ys shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya Mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Utatakiwa Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Utatakiwa Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
h) Utatakiwa Kuzingatia ratiba za shule wakati wote.
i) Utatakiwa Kutunza mali za umma, mali zako na za wenzako
j) Utatakiwa kuwa na Lugha nzuri unapoongea na wenzako au na watu wanaokuzidi umri (Lugha Za matusi, kejeli na maudhi hazitakiwi kabisa)
k) Utatakiwa kuandika notes, kufanya mazoezi na kufanya majaribio ya kila somo unalosoma.

E.2 UTARATIBU KATIKA BWALO LA CHAKULA

(a) Ni muhimu kufuata utaratibu na saa zilizopangwa za kula kufuatana na ratiba ya shule.
(b) Kila mwanafunzi awe na sahani, bakuli, kijiko na kikombe. Vyombo hivi vitunzwe bwenini.
(c) Wanafunzi wakae mezani wakati wa chakula.
(d) Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wakati wa chakula.
(e) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na ndala au kiatu cha wazi (sandals) AU kandambili ndani ya bwalo la chakula.

E.3 JIKONI

(a) Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia jikoni wala kujipikia vyakula kama wanavyotaka.
(b) Viranja wa zamu na viongozi wa meza ndio wanaoruhusiwa kuingia jikoni wakati wa kupakua chakula.

E. 4 MABWENINI

(a) Wanafunzi hawaruhusiwi kulala wawili kitanda kimoja.

(b) Kila mwanafunzi ni lazima alale katika bweni na chumba alichopangiwa.
(c) Wanafunzi hawaruhusiwi kuongea, kutembea mabwenini au nje ya bweni baada ya saa 5:00usiku.
(d) Ni marufuku kupiga na kusikiliza muziki bwenini.
(e) Upotevu/uharibifu wowote wa mali ya umma bwenini utalipwa na wakazi husika wa bweni.
(f) Mwanafunzi haruhusiwi kuwepo bwenini wakati wa masomo au wakati ratiba ya shule ikiendelea.
(g) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na chakula au kula chakula bwenini.
(h) Kila mwanafunzi azingatie usafi wa bweni siku zote na siku maalum za usafi.

E. 5 DARASANI
(a) Wanafunzi wawe madarasani mnamo saa moja na dakika hamsini asubuhi.
(b) Mwalimu anapoingia darasani wanafunzi wasimame na kuamkiana na mwalimu.
(c) Wanafunzi wasipige kelele wawapo darasani.
(d) Wanafunzi wasitoke nje ya darasa wakati wa masomo bila ruhusa maalum.
(e) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujibu na kuuliza maswali na kukamilisha kazi alizoachiwa na mwalimu wa somo.
(f) Usafi wa darasani ni wajibu wa kila mwanafunzi.

E.6 NJE YA DARASA
(a) Wanafunzi wasimame na kumsalimu mwalimu au mtu aliyewazidi umri kila anapopita.
(b) Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni kama inavyostahili.
(c) Wanafunzi watumie lugha ya heshima kwa walimu, watu wengine na hata wao kwa wao.
(d) Wanafunzi wawe watii, wasiwe wagomvi, wasengenyaji, wavivu, walevi na wazururaji.
(e) Wanafunzi wawe na moyo wa kushirikiana na kusaidiana wakati wa shida na raha.
(f) Wanafunzi waheshimu bendera ya taifa na ukumbi wa mikutano.
(g) Wanafunzi hawaruhusiwi kusomea nje ya madarasa, mabwenini au bwaloni.
(h) Mwanafunzi ataongea kiingereza wakati wote awapo shuleni.

E.7 MIPAKA YA SHULE
Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo;
(a)Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa Shule
(b)Kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum;
   i. Chumba cha walimu (staffroom)
   ii.Ofisi za Shule
   iii.Maabara
   iv.Jikoni

E.8 MATIBABU
(a) Wagonjwa wote watatibiwa Zahanati ya kijiji cha kibaoni iliyopo Kata ya kibaoni / kituo cha afya usevya pamoja na Hospitali ya Serikali ya Wilaya.
(b) Shule inatoa huduma ya kwanza tu. Gharama za matibabu ya hospitali ni ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

E.9 UGONJWA
(a)Tafadhali mzazi/mlezi unatakiwa kufanya **uchunguzi wa kina wa afya ya mwanao** kabla hajaripoti Shuleni na wakati wa likizo ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
(b)Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa Kwenye uongozi wa Shule
(c)Mwanafunzi mgonjwa mwenye matatizo lazima aufahamishe uongozi wa shule au matroni wa shule Mara afikapo shuleni.
(d)Shule haitoi chakula maalumu (special diet) kwa wanafunzi wagonjwa.

E.10 MAKTABA YA SHULE
(a) Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia maktaba wakiwa wamebeba mikoba ya vitabu/ madaftari.
(b) Wanafunzi waingie maktaba wakiwa wamevaa vazi rasmi la shule.
(c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya maktaba na kitabu au gazeti bila ruksa ya mkutubi au mwalimu mhusika na maktaba.
(d) Mwanafunzi ataingia maktaba katika muda maalumu uliopangwa tu.

E.11 WAGENI
(a) Wageni wa aina yoyote ile hawaruhisiwi kuingia au kupita shuleni bila shida maalumu na idhini ya mlinzi au mwalimu wa zamu.
(b) Wageni wa aina yoyote ile hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi isipokuwa kwa wale wenye shida za kiofisi tu kupitia kwa mwalimu wa zamu

E.12 HUDUMA ZA OFISI
(a) Ofisi ya shule ndiyo itapokea taarifa za dharura za wanafunzi kama vile msiba au tatizo kubwa la kifamilia pamoja na maagizo yote ya wazazi/walezi kwa mwanafunzi.
(b) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupokea simu bila idhini ya Mkuu wa shule.
(c) Wanafunzi wanaruhusiwa kuingia ofisi yoyote shuleni isipokuwa ni lazima wagonge/ wapige hodi kabla ya kuingia.
(d) Barua za wanafunzi zitapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atazikabidhi kwa kiranja wa zamu ili azigawe kwa wahusika.

E.13 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Kusababisha mimba ndani au nje ya Shule
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuoa au kuolewa
i) Kupata mimba, Kutoa mimba ndani au nje ya Shule.
j) Kugoma, kupanga, kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu au Line ya Simu ya mkononi au kifaa chochote kinachoashiria kuwa na simu.
m) Ubakaji
n) Utoro au Kutoka nje ya Shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule
o) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu nakadhalika
p) Kumiliki silaha ya aina yoyote
q) Kumiliki Camera yoyote
r) Kumiliki kipasha joto (heater)
s) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

E.14 MAKATAZO/MAELEKEZO MBALI MBALI UTAKAYOTAKIWA KUYAZINGATI UWAPO KATIKA SHULE HII.

i) Mwanafunzi harusiwi kuvaa kofia, heren, mikufu, khanga, bangili, pete, sketi fupi au za kubana/mipasuo. Marufuku kupaka rangi kucha au nywele, kujichubua. Yeyote atakaye patikana na haya atachukuliwa hatua kali.

ii) Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, redio, Camera, CD, DVD, mshumaa, pasi ya Umeme, Heater na silaha yoyote kama vile kisu au panga. Atakayapatikana na kosa hili atachukuliwa hatua kali sana.

iii) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mapenzi, kujuhusisha na mazungumzo ya mapenzi, kuingia kwenye vilabu vya pombe, kuingia kwenye kumbi za starehe kama vile kwenye Madisko na Video, kuandika barua za mapenzi au kupokea barua za mapenzi. Atakayepatikana na kosa hilo atachukululiwa hatua kali bila msamaha.

iv) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na lugha za matusi, kejeli, dharau na kashfa. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu anayemzidi umri akiwa amejishika kiunoni au ameweka mikono mfukoni.

v) Mwanafunzi kutofanya majaribio au mazoezi au kutokusanya kazi aliyopewa au kutoandika notes (nukuu) alizopewa na mwalimu wa somo ni KOSA KUBWA SANA. Mwanafunzi atakaye patikana na kosa hili atachukuliwa hatua kali kwa kukwamisha lengo lililomleta katika shule hii.

vi) Mwanafunzi haruhusiwi kuficha taarifa za uovu wowote aliouona au kuusikia. Kupatikana na kosa hili mwanafunzi atachukuliwa hatua kali.

vii) Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi kitabuni, katika dawati, meza, viti au kwenye kuta za majengo ya shule. Kukaidi kutii katazo hili mwanafunzi atachukuliwa hatua kali sana.

viii) Ni kosa kwa mwanafunzi kumkimbia mwalimu au mfanyakazi yeyote. Mwanafunzi atakaye patikana na kosa hili atachukuliwa hatua kali za kisheria.

ix) Mwanafunzi harusiwi kufanya udanganyifu katka mtihani wowota ule, uwe wa ndani au wa nje. Kufanya kosa hili, mwanafunzi atachukuliwa hatua kali sana.

x) Katika Shule hii kuna vikundi vya dini kama vile TYCS, ASA, CASFETA, UKWATA na TAMSA.Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu kikundi anachosali mwenzake kwa asilimia 100%. Kudharau au kukejeli kikundi anachosali mwenzako kutasababisha uchukuliwe hatua kali za kisheria bila msamaha.

xi) Wastani wa Shule ni 60% atakayepata chini ya wastani huu atapewa adhabu kali bila msamaha.

xii) Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi /mlezi yafanyike kupitia Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni

xiii) Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sharia za shule

xiv) Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa ukamilifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo

xv) Iwapo mwanao anaugonjwa unaomsumbua mara kwa mara tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia akabidhi kwa mlezi. Hii itarahisisha shule kumuhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumuhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako

xvi) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wafanya kazi wa shule bila idhini ya Mkuu wa Shule

xvii) Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana kwenye idara za masomobaada ya saa 12 jioni.

xviii) Fedha ya matumizi binafsi na nauli ya kurudia nyumbani wakati wa likizo Niwajibu wa kila mzazi/mlezi kuhakikisha kwamba anampatia mtoto wake fedha kwa ajili ya matumizi binafsi pamoja na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo.

E. 15 FOMU ZIFUATAZO ZIMEAMBATANISHWA NI MUHIMU KUZIKAMILISHA
i. Historia ya wazazi/walezi na mtoto
ii.Kukubali kujiunga na shule
iii.Fomu ya kupima afya (medical examination)

Elewa kuwa si rahisi kutunga sheria za kila kosa linaloweza kufanywa na mwanafunzi. Sheria ni mwongozo wa kumwelewesha mwanafunzi mambo ambayo haruhusiwi kuyafanya. Kitu muhimu ni kwamba kila mwanafunzi atumie akili yake na busara kuweza kujua namna gani ya kuishi na walimu pamoja na wanafunzi wenzake ili kutumia nafasi yake kujipatia elimu na kuishi kwa raha na amani katika jitihada za kujiendeleza mwenyewe, shule pamoja na taifa zima.
Kumbuka kuwa umepata bahati kubwa kuwa kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule hii, kwa hali hiyo toa mchango wako katiak kujenga msingi imara, sifa na mwenendo mzuri na maendeleo safi kwa shule yako ya sekondari ya Mizengo Pinda. Nakutakia kila la kherinkatika utekelezaji wa majukumu yako kama mwanfunzi na mwanajumuiya.

MOTO WA SHULE NI “ELIMU NI UKOMBOZI” NJOO UJIKOMBOE!

KARIBU SANA!

ALICKO J. KAMINYOGE
MKUU WA SHULE

KIAMBATA ‘A’

OORODHA YA VITABU VYA MASOMO WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI

Kwa sababu shule hii ina uhaba wa vitabu, ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini: -

a) VITABU VYA HISTORIA: -

READING LIST FOR HISTORY ONE

1. Webster J.B. The Growth of African Civilization, the Revolutionary Years of West Africa Siche 1800, Longman Press.
2. Walter Rodney, How Europe Underdeveloped Africa.
3. Hallert, R. (1983). Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.
4. July, R.W. (1992). A History of the African People, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya. 5. Illife, J. (1995). Africans, the History of the Continent. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
6. Manning, P. (1990). Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade, Cambridge University Press.
7. Njiro, E. (1989). A History of Africa in the 19 th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
8. Rodney, W. (1976). How Europe underdeveloped Africa, Publishing House, Dar es salaam, Tanzania.
9. Shillington, K. (2004). History of Africa. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.
10. Davidson, E. ef al (1997); The growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19 th century, Longman Group Limited, Singapore.
11. Freud, B. (1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, Colorado, Lynne Rienner Publishers.
12. Kimambo, I and Temu, A (1969); A History of Tanzania, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
13. Robin, H. (1993); African since 1875 A modern History, East African Publishers Ltd, Nairobi, Kenya.
14. Roland, O. and Anthony, A. (2007). Africa since 1800, Cambridge University Press, New York, USA.
15. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
16. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)
17. History for secondary schools: Form Five (TIE).
18. History for Secondary Schools: Form Six (TIE)

READING LIST FOR HISTORY TWO

19. Nelson throne Essential modern world history
20. History of 21 st century (World history) (Oxford)
21. H.L. Peacock. A History of Modern Europe 1789-1981 seventh Edition (2010)
22. The History of Modern World (2007) 6 th Edition by Oxford University Press.

b) VITABU VYA KISWAHILI: -

1. J.A. MASEBO na M. Nyangwine, Nadharia ya Kiswahili Kidato cha Tano na Sita.

2. H. J.M. Mwasiko, R.D.K. Mekacha, D.L. Masoko, P.C.K. Mtengwa; Kitanglizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu.
3. Tahakiki kidato cha tano na sita.
4. Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II.
5. Kiswahili – I: Mwandishi Masuko Christopher Saluhaya.
6. Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu. Wandishi: - H.J.M. Mwansoko, R.D.K. Makacha, S.L.W. Masoko, P.C.K. Mtengwa.
7. Kiswahili Sekondari – Kidato cha Tano (TIE)
8. Kiswahili Sekondari – Kidato cha Sita (TIE)

9. VITABU VYA UCHAMBUZI USHAIRI

Kimbunga - H. Goro
Fungate ya uhuru - M.S. Khatibu
Chungu tamu - T.A. Mvungi

RIWAYA.

Vuta n'kuvute - S.A. shafi
Usiku utakapokwisha - M. Msokile
Mfadhili - H. Tuwa

TAMTHILIYA

Morani - E. Mbogo
Nguzo mama - P. Muhando
Kivuli kinaishi - S. Mohamedi

c) VITABU VYA JIOGRAFIA:

1. Pritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman.
2. Msabila D. T (2003) Success in Geography climatology and Soil Science Dar es salaam – Afroplus Industries L.T.D.
3. Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa, Longman.
4. Kamili, A Comprehensive Approach Practical Geography For Advanced Level, Dar es salaam, Afroplus Industries.
5. Kamili, Physical Geography for Africa, Dar es salaam Afroplus Industries.
6. Msabila D.T. Physical Geography, Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.
7. Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.

d) VITABU VYA LANGUAGE (1) ONE: -

1. Nichlolus arshery, Comprehensive English Grammar New edition.
2. Michael Kadeghe, Sematics phonology and styhstics. (blue).
3. Ashel, N. (2009) Advanced Level English A Practical Approach. DSM.
4. Kadeghe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced Level (form Six) – DSM
5. Kadeghe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced Level (form five) – DSM.
6. English Language for Secondary Schools, Language & Usage – Form Five & /six (TIE) papers.
7. Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.

e) LANGUAGE (II)

1. Ashel, N. (2011), Advanced Level Literature. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.
2. Advanced Level Literature, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.
3. Achebe, A. (1966) A man of the People.

4. Ayi Kwei Armah (1968), The Beautiful Ones Are Not Yet Born.
5. Ibsen, H. (1882), An Enemy of the People, EA-DSM
6. Imbuga, FC (1976) Betrayal in the City.
7. Mirii Ngugi & Thing'ol (1982), I Will Marry When I Want, EAEP, DSM. 8
. Institute of Education, Selected Poems.
9. Mloka, C. (2007) The Wonderful Surgeon. 10. English Language for Secondary Schools, Literature & Stylistics – Form Five & Six (TIE). Paper 2.

f) GENERAL STUDIES: -
1. General studies Approach.
2. Richard, R.F. Mbalase. General Studies for Advanced Level Certificate;
3. Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3 rd Ed.
4. Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter. M. Deogratias. Understanding Advanced Level general Studies; Advance Secondary SchoolEducation;

KIAMBATA 'B'

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI, KUKUBALI SHERIA ZA SHULE NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

| *Picha ya mwanafunzi* |
|---|

A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI (Ijazwe na mwanafunzi):
1. Jina kamili la mwanafunzi ____________________________________
2. Tahasusi ______ Jinsia (Me/ Ke) _________ Uraia ________________
3. Kabila ____________Dini_______________ Kanisa / msikiti anakosali ni ________________________
4. Tarehe ya kuzaliwa ________________
5. Mahali alipozaliwa: Kitongoji/ mtaa ________________________
Kijiji ________________________ Kata ____________________ Tarafa _____________________Wilaya/Mji ____________________ Mkoa__________________ 6. Yatima / Sio yatima ___________________ Amempoteza ___________________________________
7. Historia ya Shule alizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Mizengo Pinda

(a) S/M MSINGI: JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI SHULE YA MSINGI…………………………………………… ALIKOTOKA……………………………….TAREHE NA MWAKA ALIOANZA…………………………………………… TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA/ MALIZA……………………………………

1. (B) SEKONDARI:
JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI SHULE YA SEKONDARI………………………………….. TAREHE NA MWAKA ALIOANZIA……………………………………… TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA/ MALIZA………………………………… 8. Namba ya Mtihani (CSE); ________________ Shule niliyofanyia kidato cha nne; _______________ Wilaya ya _________________________________ Mkoa wa

---

B. KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA.
MIMI…………………………………………KIDATO CHA…………MWAKA…..……… .MCHEPUO WA……………
Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea/ sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.
TAREHE:…………………………………. SAINI: ……………………………

C. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:
MWANAFUNZI:
Mimi: ………………………............................................................ wa Tahasusi ya …………nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria, kanuni, taratibu, miongozo ya
shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa
Tarehe…………………………………..Saini…………………………………

D. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI ;( ANDIKA MAJINA MATATU)

*Picha ya baba*

1. JINA LA BABA: ……………………………...................................................
JE, BABA YUKO HAI/AMEFARIKI: ……………….………
MAHALI ANAPOISHI:
KITONGOJI:…………………….….KIJIJI:……………………..KATA:………………………
TARAFA ……………......... WILAYA ………………………: KAZI YA BABA:…….................................. SIMU YA BABA ............................................ S.L.P......................... MJI.........................................

*Picha ya Mama*

2. JINA LA MAMA…………………………..................................................
YUKO HAI/AMEFARIKI …………………………
MAHALI ANAPOISHI:
KITONGOJI………………………KIJIJI……………………………KATA……………
TARAFA…………..WILAYA………………………..
KAZI YA MAMA: ………............. SIMU YA MAMA..........................................S.L.P.......................... MJI......................................

ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI (Ajaze sehemu)

*Picha ya mlezi wa kiume*

3. JINA LA MLEZI WA KIUME…………………………..……….……
MAHALI ANAPOISHI.................................UHUSIANO..............................
SIMU:...............................S.L. P ……………… MJI ………………
KAZI ANAYOFANYA …………………………………… MWAJIRI ……………………………

*Picha ya mlezi wa kike*

4. JINA LA MLEZI WA KIKE..........................................................
MAHALI ANAPOISHI ...........................UHUSIANO..............................

SIMU............................S.L.P............................ MJI.............................
KAZI ANAYOFANYA ………………………………. MWAJIRI ……………………….

E. MZAZI/MLEZI (Azaje Sehemu Hii):

Mimi………………………………………. nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi…………………………………………na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri. Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo. TAREHE:……………… SAINI: ………………………………

F: SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU:

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi anapokuwa shuleni.
Majina matatu mfano: ROSE ZABRON MUSSA.

| JINA | UHUSIANO | NAMBA ZA SIMU: |
| --- | --- | --- |
| 1. ……………………………….............. | ………………………… | ………………………………….. |
| 2. ………………………………................. | …………………………... | ..................................... |
| 3 ………………………………................. | …………………………... | ..................................... |
| 4.………………………………................. | …………………………... | ..................................... |

KIAMBATA ‘C’

THE REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MPIMBWE DISTRICT COUNCIL

PART A
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION
TO: Medical Officer FROM: THE HEADMASTER
MIZENGO PINDA SECONDARY SCHOOL.
P O BOX 607
MPANDA-KATAVI

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time academic studies.
A: 1. (a) Eye –sight (b) Hearing (c) Speech (d) Veneral Disease (e) Leprosy (f) Limbs (g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases
B: BLOOD GROUP______

PART: B FOR MEDICAL EXAMINATION
(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time academic studies at your school.
(a) Eye-sight……………………………………………………………………………..……
(b) Hearing …………………………………………………………………………………
(c)Speech…………………………………………………………………………………
(d) Veneral disease………………………………………………………………………….
(e) Leprosy …………………………………………………………..………………………..
(f) Limbs ………………………………………………………………………………….
(g)Epilepsy…………………………………………………………………………………
(h)Neurosis…………………………………………………………………………………
(i) Pregnancy ……………………………………………..…………………………………
(j) Other serious diseases…………………………………………..…………………………
(k) BLOOD GROUP ……………………………………………………………………………

DATE………………… SIGNATURE ……………………… OFFICIAL STAMP………………